# Tiba ya Mtandaoni katika *Mpango wa Watoto Wachanga wa NC (N.C. ITP)*



## Tiba ya mtandaoni ni nini?

- Tiba ya mtandaoni ni utoaji wa tiba "pepe" kwa kutumia simu, kompyuta binafsi au tableti, wakati daktari yuko mbali na familia.
- Tiba ya mtandaoni itashughulikia matokeo yaliyotambuliwa na familia kwenye Mpango wa Huduma Binafsi ya Familia (IFSP, Individualized Family Service Plan).




## Tiba ya mtandaoni hufanyikaje?

- Tiba ya mtandaoni hutumia teknolojia, kama vile kompyuta za binafsi, tableti na simu mahiri kuunganisha madaktari na familia. Vipindi vya tiba "hutiririshwa," kwa kutumia Wi-Fi au data ya mtandao wa simu.
- Daktari wako atakutumia kiungo salama kupitia barua pepe kwenye kifaa chako. Ukibofya kiungo hicho utaunganishwa na daktari.
- Daktari wako anaweza kupanga kipindi cha majaribio kwanza ili kuhakikisha unaweza kuunganishwa bila matatizo.
- Mara za kupokea tiba ya mtandaoni itategemea mahitaji binafsi ya mtoto wako.
- Wakati mwingine unaweza kuchagua vipindi vya tiba ya mtandaoni na ya ana kwa ana, kulingana na mapendeleo yako na mahali alipo daktari wako.

## Familia huanzaje kushiriki?

- Ikiwa familia na timu ya mpango wa IFSP waliamua kuwa mtoto wako anaweza kufaidika kutokana na tiba hiyo, Mratibu wa Huduma za Suluhu za Mapema atatoa huduma za tiba ya mtandaoni kama chaguo.
- Huenda ukahitaji kuhakikisha na bima yako ili uone ikiwa tiba ya mtandaoni ni huduma inayolipiwa na bima.

## Tiba ya mtandaoni ni salama na ya siri?

- Ndiyo. Watoa huduma za tiba ya mtandaoni hufuata kanuni za usiri zinazofuatwa na wale wanaotoa huduma za ana kwa ana.
- Shirika la Huduma za Maendeleo ya Watoto (CDSA, Children's Developmental Services Agency) huhakikisha kuwa faragha ya maelezo ya afya ya familia inalindwa.



ukijua
**mapema,**
atakua
**vizuri!**

NC DEPARTMENT OF
**HEALTH AND HUMAN SERVICES**
Division of Child and Family Well-Being
NC Infant-Toddler Program (NC ITP)

# Je, tiba ya mtandaoni inafaa kwa mtoto na familia yako?

## *Mpango wa* Watoto Wachanga wa North Carolina



- ☐ Una muunganisho wa intaneti wa kutegemewa au muunganisho mzuri wa mtandao wa simu na data isiyo na kikomo?
- ☐ Una tableti au laptopu? Ni rahisi vipindi vikifanyika kwenye skrini kubwa, lakini pia simu mahiri inaweza kutumika.
- ☐ Una anwani ya barua pepe ambapo daktari anaweza kukutumia kiungo cha kipindi?
- ☐ Unafurahia kutumia kifaa chako (laptopu, tableti au simu mahiri)?

## Mbona nichague tiba ya mtandaoni?

- Tiba ya mtandaoni inakuwezesha upokee huduma katika maeneo ambako madaktari hawapatikani.
- Tiba ya mtandaoni inakuruhusu ufikie madaktari wenye ujuzi maalum ambao huenda hawapatikani mahali ulipo.
- Wazazi wengi wanapendelea tiba ya mtandaoni.
- Tiba ya mtandaoni hufanya kazi vizuri kwa watoto wenye aibu au wanaowaogopa wageni.

## Kipindi cha tiba ya mtandaoni hufanyikaje?

1. Wewe na daktari mtajadiliana jinsi ambavyo umeendelea tangu kipindi kilichopita cha tiba ya mtandaoni na kuamua mtakachokishughulikia siku hiyo.
2. Daktari atapendekeza shughuli na mikakati ya kujaribu na mtoto wako kisha atakuchunguza wewe na mtoto wako mkifanya shughuli.
3. Daktari atakupa maoni na mapendekezo.
4. Mtajadili kilichofanya kazi vizuri siku hiyo, na mtakachojaribu nyumbani kabla ya kipindi kinachofuata.



## Tiba ya mtandaoni ni ya mtoto NA mzazi.

- Watoto wadogo *hawatarajiwi* kuketi kwa utulivu na kuangalia skrini.
- Badala yake, utacheza na kuzungumza na mtoto wako, daktari anapokufunza jinsi ya kutumia mikakati ya kuboresha ujuzi wa mtoto wako.
- Tiba ya mtandaoni hutumia vifaa ambavyo tayari unavyo nyumbani. Hakuna vifaa maalum vinavyohitajika.
- Tiba ya mtandaoni italenga kumsaidia mtoto wako kujifunza wakati wa shughuli zake za kila siku, kama vile wakati wa kula, wakati wa kucheza, kuingia kwenye gari au hata wakati wa kuoga.
- Wazazi na wanafamilia nyumbani hushirikiana mara nyingi zaidi na watoto wao na ni walimu wao muhimu zaidi!

NC DEPARTMENT OF
HEALTH AND
HUMAN SERVICES
Division of Child and Family Well-Being
NC Infant-Toddler Program (NC ITP)

# Maoni ya mzazi kuhusu tiba ya mtandaoni



- *Ninapenda urahisi wa tiba ya mtandaoni! Mtoto wangu msichana ana aibu, kwa hivyo inamsaidia sana. Anaweza kushiriki kwa muda anaopenda na kuondoka. Kama haingekuwa tiba ya mtandaoni, hatungeweza kupokea huduma.*
- Tiba ya *mtandaoni ilimwezesha mtoto wangu kupata msaada aliohitaji, na kwa kweli ameendelea vizuri. Ameimarika zaidi tangu alipojiandikisha katika mpango huo!*
- *Ninapendelea tiba ya mtandaoni kwa sababu nyingi, na inaendana na ratiba yangu vizuri kabisa.*
- *Mtoto wangu anafurahia zaidi tiba ya mtandaoni. Yuko huru katika mazingira yake binafsi na amezoeana na daktari kwa mbali.*
- *Nilipenda ushauri wa kutumika katika shughuli za kawaida. Mambo mengi ambayo sikuwa hata nimefikiria kuyashughulikia yalinisaidia!*
- *Kujaribu mikakati katika wakati halisi na tiba ya mtandaoni ndiko kulikosababisha tupige hatua.*
- *Nilipenda urahisi wa kubadilika kwa ratiba ya siku na saa.*
- *Daktari wangu wa mtandaoni amekuwa mwenye maarifa zaidi na hufafanua mambo kwa njia tunazoelewa na kutumia kila siku na mtoto wetu mvulana.*
- *Nilipenda kuweza kujaribu ratiba na shughuli katika wakati halisi, na maoni.*
- *Ninapenda sana urahisi wa kutumia tiba ya mtandaoni! Daktari wa mtandaoni atanitumia kiungo kupitia barua pepe. Kisha nitabofya kiungo hicho na tutamwona naye atatuona!*



ukijua
**mapema**,
atakua
**vizuri**!


**Idara ya Afya na Huduma za Binadamu ya • North Carolina •** www.ncdhhs.gov
**Sekta ya Ustawi wa Watoto na Familia • Kitengo cha Suluhu za Mapema •** www.beearly.nc.gov
N.C. DHHS ni mwajiri na mtoa huduma asiyebagua mtu yeyote. 6/22, 1/23

NC DEPARTMENT OF
**HEALTH AND HUMAN SERVICES**
Division of Child and Family Well-Being
NC Infant-Toddler Program (NC ITP)